



## State of Michigan Attorney General Dana Nessel

### **ITOLWE MARA MOJA:**

Alhamisi, Machi 26, 2020

### **TAHADHARI MUHIMU KWA WATUMIAJI: Ulaghai wa Malipo ya Msaada wa Serikali**

Wakili Mkuu wa Michigan Dana Nessel alitoa tahadhari ya haraka ya watumiaji kuwahimiza wakazi wa Michigan kuwa wanalifu kuhusu waigizaji wabaya wenye nia ya kuwashurutisha kutoa habari zao za kibinafsi katika mpango wa serikali wa kutoa msaada.

Walaghai wanatumia habari kwamba serikali ya federali itatuma malipo ya wakati- mmoja kwa mamillioni ya watu kote nchini kama sehemu ya uchumi wa shirikisho nafuu kwa kujibu COVID-19 ili kuiba habari za kibinafsi.

Idara ya Wakili Mkuu wa Michigan tayari imeshapokea ripoti kwamba wakaazi wanapata barua pepe kutoka tovuti zinazoonekana kuwa za kiofisi wakidai wanatoa PayPal, akaunti za beki, au habari nyinginezo za kifedha ili kupokea \$1,200 malipo ya kichocheo cha serikali mara moja.

Ukipokea ujumbe wa simu, barua pepe au simu kutoka kwa mtu anayesema kuwa yeye anatoka serikalini na cheki yako—**USISADIKI.**

Kashfa hizi za bandia za uwongo hupendelea kuuliza habari ya akaunti yako ya benki na kusisitiza ya kwamba \$1,000 au zaidi zitawekwa moja kwa moja kwenye akaunti yako ya benki.

**Kaa macho:** Usikubali, kwa hali yoyote, kutoa habari yako ya kibinafsi kupitia, ujumbe wa simu, barua pepe, au simu.

**Unawezaje kuwa na hakika kuwa ni ulaghai? Zingatia ishara hizi:**

**Ombi lolote la malipo.** Hakuna malipo ya mbele, ada, au malipo ya aina yoyote ili kupokea malipo ya msaada kutoka kwa serikali. Hutaaulizwa kulipa pesa yoyote, pamoja na “ada ya usindikaji.” Mtu yeyote anayedai kuwa anatoka kwa serikali ya federali, ya jimbo, au serikali ya mtaa anayeuliza malipo yoyote ni mlaghai. Usijibu aina yoyote ya mawasiliano iwapo utaulizwa malipo ya aina yoyote. **Kumbuka:**

walaghai tu ndio watakuuliza malipo ili kupokea msaada kutoka kwa serikali. Usikubali kulaghaiwa!

**Ombi lolote la habari ya kibinafsi au ya kifedha.** Serikali haitakupigia simu au kukutumia ujumbe wa simu ili kuhakikisha au kuuliza nambari yako ya Usalama wa Jamii (Social Security number), akaunti ya benki, au nambari ya kadi ya mkopo ili upewe msaada wa kifedha. Usiingize habari yako ya kibinafsi au ya kifedha kwa kujibu barua pepe, ujumbe wa simu, au kurasa za wavuti zinazoonekana kama kwamba ni za serikali ya federali. Walaghai tu ndio watakaosisitiza w utoe habari zako za kibinafsi – Nambari ya Usalama wa Jamii, nambari za akaunti ya benki, kadi yako ya mkopo, au pini – ili upate msaada wa kifedha.

**Msaada wowote wa kukusaidia kuomba kupokea msaada wa kifedha. Kwa uhakika** hakuna mchakato wowote wa maombi wa msaada ya kifedha ya aina yoyote. Malipo yatafanywa moja kwa moja kupitia akaunti ya benki moja kwa moja au kwa kupitia cheki itakayotumwa nyumbani kwako. Mtu atakayekuambia anaweza kukusaidia kuomba pesa hii ni mlaghai.

**Kutolewa kwa ruzuku yoyote inayohusiana na malipo haya** waigizaji wabaya wanaweza kuacha ujumbe wakiulizia habari ya kibinafsi au ya kifedha ili kukuharakishia kupata fedha ya msaada kwa upesi kupitia ruzuku au uthibitisho wa kitambulisho ili kupokea fedha hizo. Kwa njia nyingine, walaghai wanaweza kuahidi ufadhili wa ziada zaidi ya kiwango cha msaada wa serikali kwa ubadilishaji ya malipo ndogo au habari ya kibinafsi. Hakuna pesa zozote za ruzuku kama hizo.

Pia hakikisha ya kuwa **haufungui kamwe kiambatisho au viungo vilivyotumwa** kutoka kwa mtu yeyote anayedai kuwa anatoka serikalini. Usijibu na kufuta ujumbe huo mara moja.

**Kwa habari sahihi zaidi na ya kisasa kuhusu msaada ya kifedha kutoka kwa serikali ya federali na maelezo maalum ya ulipaji, tembelia [tovuti ya IRS](#) tu**